Maisha Yaliyojaa Wimbo (A Song-Filled Life)

Na

Terry Warford

Maisha Yaliyojaa Wimbo

Na

Terry Warford

Novemba 5, 2011

Maisha Yaliyojaa Wimbo

Zaburi 100: 1-2, "*Mfanyieni BWANA shangwe, dunia yote; mtumikieni BWANA kwa furaha; njooni mbele zake kwa kuimba;*"

Kuimba ni moja ya furaha kuu katika maisha, inaleta furaha kwetu na pia kwa Baba yetu aliyembinguni. Katika jarida hili, tunataka kuangalia jinsi gani tunavyojaza maisha yetu na nyimbo. Tujifunze ni wakati gani tofauti tunaweza kuimba, sababu ya kuimba, na baraka ambazo nyimbo huleta katika maisha yetu. Alafu tutahitimisha na vipengele muhimu ambazo hazikuwa sehemu nyingine.

Tuanze na nyakati tofauti tunazoweza kuimba.

Kwanza kabisa, kuimba ni sehemu ya ibada yetu. Katika sura ya 14 ya 1 Wakorintho, Paulo anajibu maswali mengi ambayo Wakorintho wanauliza kuhusu ibada. Katika msitari wa 26, anaeleza kwamba kuimba ni sehemu ya tendo hilo, "*Basi ndugu imekuaje? Mkutanapo pamoja kila mmoja ana zaburi, ana fundisho, ana ufunuo, ana lugha, ana tafsiri. Mambo yote na yatendeke kwa kusudi la kujenga.*" Na katika Ebr. 2:12, "*Akisema, nitalihubiri jina lako kwa ndugu zangu, katikati ya kanisa nitakuimbia sifa.*"

Hataivyo, hatujawekewa ukomo wa kuimba siku za ibada tu. Meza ya Bwana na matoleo hutafsiriwa kwa mfano na agizo katika siku ya kwanza ya juma. Lakini tuweza kuimba wakati wo wote tunaotaka. Awali ya yote, Paulo na Sila waliimba usiku wa manane gerezani. Mdo. 16:23-25, "Na walipokwisha kuwapiga mapigo mengi, wakawatupa gerezani, wakamwamuru mlinzi wa gereza awalinde sana. Naye akiisha kupata amri hii akawatupa katika chumba cha ndani, akawafunga miguu kwa mkatale. Lakini panapo usiku wa manane Paulo na Sila walikuwa wakimwomba Mungu na kumwimbia nyimbo za kumsifu, na wafungwa wengine walikuwa wakiwasikiliza." Hivyo tunaweza kuimba wakati wo wote tunaotaka.

Kwa vile hili ndilo swala, hebu na tuimbe nyimbo za kumsifu Mungu kila siku. Ebr. 13:15, "*Basi kwa njia yake yeye na tumpe Mungu dhabihu ya sifa <u>daima</u>, yaani tunda la midomo iliungamayo jina lake.*" Zaburi 145:2, "*Kila siku nitakuhimidi, nitalisifu jina lako milele na milele.*"

Kuna sababu nyingi za sisi kuimba. Hebu tuangalie chache.

Kwanza, tunaimba ili kumsifu Mungu. Zab. 147:1, "*Haleluya msifuni Bwana, maana ni vyema kumwimbia Mungu wetu, maana kwapendeza kusifu ni kuzuri.*" Zab. 98:4, "*Mshangilieni BWANA nchi yote, inueni sauti, imbeni kwa furaha, imbeni zaburi.*"

Tunamwimbia Mungu zaburi kwa sababu tunashukurani kwake. Efe. 5:19-20, "*Mkisemezana kwa zaburi na tenzi na nyimbo za rohoni, huku mkiimba na kumshangilia Bwana mioyoni mwenu; na kumshukuru Mungu Baba siku zote kwa mambo yote, katika jina lake Bwana wetu Yesu Kristo.*"

Pia tunaimba kama mfumo wa kufundisha moja na mwingine. Kol. 3:16, "*Neno la Kristo na likae kwa wingi ndani yenu katika hekima yote, mkifundishana na kuonyana kwa zaburi, na nyimbo, na tenzi za rohoni; huku mkimwimbia Mungu kwa neema mioyoni mwenu.*"

Tunaweza pia kutumia nyimbo kama njia ya kufundisha ulimwengu. Zab. 96:1-3, "*Mwimbieni BWANA wimbo mpya, mwimbieni BWANA nchi yote. Mwimbieni BWANA libarikini jina lake, tangazeni wokovu wake siku kwa siku. Wahubirini mataifa habari za utukufu wake, na watu wote habari ya maajabu yake.*"

Pia tunaimba kuufikia uwepo wa Mungu, kama tulivyosoma katika Zab. 100: 2, "*Mtumikieni BWANA kwa furaha, njooni mbele zake kwa kuimba.*"

Kumwimbia Mungu nyimbo za sifa hubariki maisha yetu kwa njia nyingi.

Nyimbo huleta furaha kuu katika maisha yetu. Zab. 33:1, "*Mpigieni BWANA vigelegele, enyi wenye haki, kusifu kunawapasa wanyofu wa moyo.*" Yakobo 5:13, "*Mtu wa kwenu amepatikana na mabaya? Na aombe. Ana moyo wa kuchangamka? Na aimbe zaburi.*" Nimewahi kuulizwa swali: je, tunaimba kwa sababu tunafuraha, au tunafuraha ndio maana tunaimba? Kiukweli, kulingana na maandiko majibu yote ni sahihi.

Nyimbo huleta faraja katika wakati mgumu wa maisha. Angalia Mat. 26:30, wakati Yesu alikuwa anakaribia kufa. Hii ilikuwa ni mara baada ya kuanzisha meza ya Bwana, lakini kabla hajaenda Gethsemani kuomba. "*Nao walipokwisha kuimba, wakatoka nje kwenda mlima wa mizeituni.*" Tunapaswa kuwa makini, hataivyo. Faraja kama hii kupitia nyimbo haiwezi kulazimishwa kwa wengine, inapaswa kutoka ndani. Angalia Mithali 25:20, "*Amwimbiaye nyimbo mtu mwenye moyo mzito, ni kama yeye avuaye nguo wakati wa baridi; ni kama siki juu ya magadi.*" Moja ya kifungu kinachovutia katika biblia ni Zaburi 137:1-4, *"Kando ya mito ya Babeli ndiko tulikoketi tukalia tulipoikumbuka Sayuni. Katika miti iliyo katikati yake, tulivitundika vinubi vyetu. Maana huko waliotuchukua mateka walitaka tuwaimbie; na waliotuonea walitaka furaha; tuimbieni baadhi ya nyimbo za Sayuni. Tuuimbeje wimbo wa BWANA katika nchi ya ugeni?*" Hivyo hatuwezi kulazimisha faraja kupitia nyimbo. Lakini kama inatoka ndani, nyimbo zinaweza

kuwa chanzo cha faraja. Zab. 77:6, "*Nakumbuka wimbo wangu usiku, nawaza moyoni mwangu, Roho yangu ikatafuta.*"

Kuimba ni njia kuu ya kuwa na ushirika na wengine. Zab. 34:3, "*Nalimtafuta BWANA akanijibu, akaniponya na hofu zangu zote.*" Na kama tulivyosoma katika Ebr. 2:12, "*Akisema, nitalihubiri jina lako kwa ndugu zangu; katikakati ya kanisa nitakuimbia sifa.*"

Kuimba pia ni njia kuu ya kuwa na ushirika na Mungu. Zab. 100:4, "*Ingieni malangoni mwake kwa kushukuru; nyuani mwake kwa kusifu; mshukuruni, mhimidini jina lake.*" Zab. 22:3, "*Na wewe U mtakatifu, uketiye juu ya sifa za Israeli.*"

Kwaiyo, maisha yetu yanaweza kujaa nyimbo kwa kuimba wakati wa ibada, kuimba wakati wo wote, na kila siku. Tunaimba kwa sababu nyingi, pamoja na kumsifu Mungu, nje ya kumshukuru, kufundisha mmoja baada ya mwingine, kuifundisha ulimwengu, na kuufikia uwepo wa Mungu. Kuimba hubariki maisha yetu katika njia nyingi; kwa furaha, kwa furaha na faraja katika nyakati ngumu, ikiwa tu faraja huja kupitia nyimbo kutoka ndani na siyo kwa lazima. Kuimba pia ni baraka kwa maana kwamba ni njia kuu ya kuwa na ushirika kwa mmoja na mwingine, na Mungu.

Tuhitimishe kwa kwa vipengele viwili kwa haraka.

Kwanza, tunapaswa kuhakikisha kwamba tunaimba nyimbo za kimaandiko. Zab. 47:7, "*Maana Mungu ndiye mfalme wa dunia yote, imbeni kwa akili.*" Kol. 3:16, "*Neno la Kristo na likae kwa wingi ndani yenu katika hekima yote, mkifundishana na kuonya kwa zaburi, na nyimbo, na tenzi za rohoni; huku mkimwimbia Mungu kwa neema mioyoni mwenu.*" Zab. 119:54, "*Amri zako zimekuwa nyimbo zangu, katika nyumba za ugeni wangu.*"

Mwisho, tunapaswa kuhakikisha kuwa tunajenga juu ya Ukristo wetu nyimbo pamoja na kuishi maisha ya Ukristo. Tusifanye nyimbo zetu kuwa bure ya kinafiki. Tuishi kama jinsi tunavyoimba. Angalia jinsi Waisraeli walivyoshindwa kufanya hivyo baada ya kuokolewa na Mungu kutoka utumwani Misri. Zab. 106:11-14, "*Maji yakawafunika watesi wao, hakusalia hata mmoja wao. Ndipo walipoyaamini maneno yake, waliziimba sifa zake. Wakayasahau matendo yake kwa haraka, hawakulingojea shauri lake. Bali walitamani sana jangwani, wakamjaribu Mungu nyikani.*" Tusiwe kama Waisraeli. Badala yake, tujenge juu ya uimbaji wetu pamoja na kuishi maisha ya Ukristo. Ebr. 13:15-16, "*Basi kwa njia yake yeye na tumpe Mungu dhabihu ya sifa daima, yaani tunda la midomo iliungamayo jina lake. Lakini msisahau kutenda mema na kushirikiana;* (ushirika na wengine) *maana sadaka kama hizi ndizo zimpendezazo Mungu.*"

Katika upendo wa Wakristo,
Terry Warford.